**Mkulima Mahiri**



Bwana Loko alikuwa mkulima mahiri. Alikuza mahindi katika shamba lake. Aliyavuna mahindi katika msimu wa kiangazi. Aliyaondoa mahindi kwenye mabunzi na kuyaanika juani kwa wiki kadhaa ili yakauke. Baada ya kukauka, aliyahifadhi katika magunia maalumu na kuyaweka katika ghala.

Pindi tu alipomaliza kuyahifadhi mahindi hayo, Bwana Loko alikuwa akililima tena shamba lake. Mara kwa mara, aliwahusisha vibarua ambao walilima na kuyatayarisha shamba. Kazi hiyo ilifanyika vizuri wakati wa kiangazi.

Vilevile, katika msimu wa kiangazi, Bwana Loko alikuwa akiuondoa udongo kutoka kwenye mitaro. Mitaro hiyo ilizuia mmomonyoko wa udongo shambani msimu wa masika.

Msimu wa masika ulizipisha shughuli nyingine. Bwana Loko alizipanda mbegu za mahindi pindi mvua ilipoanza kunyesha. Mihindi ilipomea, alipalilia ili kuyaondoa magugu. Vilevile, aliiongeza mimea yake mbolea ili inawiri.

Msimu wa masika ulifuatwa na kipupwe. Wakati huo, mahindi ya Bwana Loko yalikuwa yamekomaa. Yalibaki tu kukauka. Bwana Loko aliyavuna baadhi ya mahindi yakiwa mabichi na kuwauzia wafanyabiashara. Mara kwa mara, msimu huo wa baridi kali uliandamana na manyunyu. Wakati kama huo, Bwana Loko alikuwa akiipanda mimea kama vile ya sukumawiki.

Bwana Loko alizingatia hali ya anga katika kilimo chake. Wakati wa msimu wa vuli, alipanda aina ya mihindi ambayo ilihitaji muda mfupi kukomaa.